KISWAHILI LUGHA

Kutoka swali 1 hadi 15, umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.

____1_____kweli ni ____2_____watoto wa kike ____3_____tohara, basi sitamani kuwa mwafrika halisi ____4_____,hapo ndipo palipokoleza visa vya ____5_____wasichana.

Mbona tusifuate ____6_____misahafu?Ni wavulana tu wanaostahili kukiona kisu cha ____7_____. Ndiko kusema kuwa ____8_____walioandika maandiko walikanyaga ____9_____? Kwanza, asili ____10_____jambo hili ni gani? Mbona wasiwepo watu wa kusimama ____11_____kuzitetea haki za wasichana? Tukiendelea hivi, ____12_____kuyaokoa maisha ya ____13_____wanaokufa kwa kupoteza damu____14__ fedheha____15_____!

1. A. Ama	B. Ati	C. Kama	D. Kuwa
2. A. shariti	B. sharti	C. charti	D. si budi
3. A. wapashe	B. wabishwe	C. wapishwe	D. wapashwe
4. A. mbali	B. bali	C. kwani	D. ama
5. A. kuwatahiri	B. kuwatairi	C. kuwatahayiri	D. kutaiirisha
6. A. wasemavyo	B. yasemavyo	C. zisemavyo	D. isemavyo
7. A. saisi	B. ngariba	C. sogora	D. mchinjaji
8. A. watume	B. mitume	C. watumwa	D. wahenga
9. A. chelele	B. chechele	C. kichechele	D. chelechele
10. A. za	B. la	C. na	D. ya
11. A. kiwete	B. kisota	C. kidete	D. kisheria
12. A. hatutamudu	B. tutamudu	C. tutayamudu	D. hatutayamudu
13. A. binti	B. kina binti	C. mabinti	D. akina binti
14. A. mingi	B. nyingine	C. zingine	D. nyingi
15. A. ilioje	B. iliyoje	C. zilioje	D. lililoje

Kutoka swali la 16 - 30, jibu kulingana na maagizo.

16. Mtu anapotafuna ganda la muwa ili kutoa maji yale yote na kutupa ganda tutasema
    A. anamumunya
    B. anamumucha
    C. anamaliza
    D. anatafuna.
17. Alama ifuatayo inaitwaje? (;)
    A. Nukta koma B. Nukta kituo
    C. Koloni D. Nukta.
18. Mtu mwenye miguu iliyopinda kwa ndani huitwa_____
    A. matege B. mang'ombo
    C. kiguu D. magutao.
19. Jeptoo ni mwanafunzi mpole kama_____
    A. kasuku B. njiwa
    C. maji ya mtungi D. chiriku.
20. Kiwakilishi cha nafsi katika sentensi ifuatayo ni: Ng'ombe atauzwa sokoni kesho.
    A. a B. ng'ombe
    C. atauzwa D. kesho.
21. Watu wanapoandaa c kula huvaa ____ juu ya nguo ili kuzizuia zisic afuke
    A. surupwenye B. kimoni
    C. ovaroli D. bwelasuti.
22. "Kabla ya kuondoka alituaga vizuri." Taja kihusishi katika sentensi hii.
    A. kabla ya B. kuondoka
    C. alituaga D. vizuri.
23. Bafu _____kuogea huchafuka haraka sana
    A. ya B. la
    C. cha D. mwa.
24. Kanusha sentensi hii;
    "*Mtalii amewasili na tumempokea*".
    A. Mtalii hajawasili na hatujampokea
    B. Mtalii hatawasili wala hatutampokea
    C. Mtalii asipowasili hatutampokea
    D. Mtalii hajawasili wala hatujampokea.
25. Kama umeshughulikia moto hadi ukawaka tutasema umeufanyaje?
    A. Umeuokoa. B. Umewaka.
    C. Umeukoka. D. Umeupoza.
26. Kijakazi wa Kiptum anateswa mno lakini ana uvumilivu. Kiunganishi ni_____
    A. wa B. mno
    C. ana D. lakini.
27. Majira ya mvua haba au fupi huitwaje? Haba ni_____
    A. kielezi. B. kiulizi.
    C. kivumishi. D. kihusishi.

28. Ni yupi kati ya hawa si mdudu? Kiulizi katika sentensi hii ni_____
A. yupi B. hawa
C. kati D. si.

29. Ni nani asiyehusika na habari za majini katukatu?
A. Sarahangi B. Nahodha.
C. Mwanapwa. D. Mutribu.

30. Neno "taji" ni la ngeli gani?
A. I - ZI.
B. LI - YA.
C. U - ZI.
D. I - I.

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 hadi 40.

Umewahi kuketi ukawaza na kuwazua kuhusu hatima ya dunia hii? Ukiulizwa kuhusu hatima hiyo jibu lako litakuwa lipi? Unaona kuna raha au karaha? Wewe hapo ulipo, unajiandaa kuukubali mwisho wa dunia hii ama unajitia hamnazo?

Ukweli ni kwamba, dunia inaelekea ukingoni. Haisha nasi wakazi wake tutashangaa wala hatutashangilia. Ingawa wengine wamezama katika miradi ya kujilimbikizia mali,inawapasa kutubu kila siku na kuomba bila kukoma. Ipo kila dalili ya kuisha kwa dunia hii. Mara utasikia moto umeyaharibu mali wala chanzo chake hakijulikani ngo! Mara ajali imewaua watu thelathini barasteni,mara ardhi imeporomoka kutokana na zisizojulikana ikawameza watu! Mara ni kiangazi!mara ni ukame unaofisha watu!

Wewe uanyeshikilia kuwa unaponda raha una maana gani? Kwako kiangazi na kifo ni raha? Zilizala ni starehe? Starehe ya wapi? Huu ni wakati wa kila mmoja wetu kujibidiisha kimaombi ili sote tufikie toba. Si wakati wa kuoa wake sita, saba au hata kumi. Wala si wakati wa kubadilisha wanaume kama nguo. Kimbilio ni kwa Mwumba, tusali tusamehewe dhambi ili tusije kujuta Mungu wetu atakaporejea. Ni hakika atakaporejea wengi watalia na kusaga meno.

31. Kwa mujibu wa aya ya kwanza, ni wazi kuwa mwandishi_____
A. anatafuta mali kwa hali na mali
B. anafurahi kuwa duniani
C. ni kafiri wa hali ya juu
D. anawatahadharisha waja kuhusu mwisho wa dunia.

32. "Kujitia hamnazo" kama ilivyotumika kwenye habari lina maana ya _____
A. kutojali
B. kutaka kupata kitu
C. kufahamu baadaye
D. kushika huku na huko.

33. Kujilimbikizia mali inamaanisha nini?
A. Kutumia mali ovyo ovyo bila kujali.
B. Kujiwekea kidogo kidogo hadi yawe mengi.
C. Kuiba mali ya wengine ili watajirike.
D. Kufanya bidii kuwa tajiri.

34. Habari za kutubu kwa mfuasi yeyote
A. ni jambo la kila siku
B. ni jambo la kila ombi
C. ni jambo la siku ya hatima
D. ni jambo la kushughulikiwa.

35. Ni mangapi yaliyotajwa kuonyesha taashira za kuisha kwa dunia?
A. Saba.
B. Matatu.
C. Matano.
D. Hatujaelezwa lakini ni mengi.

36. Katika aya ya tatu, watu wengine_____
A. wanaponda raha tu
B. hawana shida maishani
C. hufurahia kiangazi kijapo
D. hawajali majanga ya wenzio mradi wametosheka kimaisha.

37. ***Zilizala***, ni
A. Mshtuko wa damu
B. Mtetemeko wa ardhi
C. Janga la angani
D. Mambo yaliyopita.

38. Inaonekana kuwa suala la kuoa wake wengi au kubadilibadili waume ni_____
A. utomvu wa maadili
B. utovu wa maadili
C. utajiri wa mtu
D. kawaida ya maisha.

39. Neno "dhambi" limepigiwa mstari lipo kwenye ngeli gani?
A. I - ZI.
B. I - I.
C. U - YA.
D. LI - YA.

40. Chagua kichwa bora kitakachoufaa ufahamu uliosoma.
A. Majanga mbalimbali
B. Ishara za siku ya kiama
C. Mitetemeko ya ardhi
D. Dhambi na madhara yake.

Compiled and supplied online by Schools Net Kenya | P.O. Box 85726 – 00200, Nairobi |
Mob. 0711 8822 27 | Email: infosnkenya@gmail.com | Order answers online at www.schoolsnetkenya.com

Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 41 hadi 50

Yamezuka mambo sufufu ambayo yakini hayakutarajiwa tangu dunia kuumbwa. Mambo hayo hayahesabiki. Yamewashangaza mashaibu na maajuza ambao hawajafa. Hata sisi tunapoyaona, tunashindwa tufiche wapi vichwa vyetu na macho ili tusione!

Haipo haja ya kuelezea jinsi wasichana wanavyotembea uchi tena kwani, limekuwa jambo la kawaida wala si ajabu tena. Jambo ambalo limenishinda na kunisinya ni shetani aliyewaingia vijana wavulana. Utasema nini unapowaona wavulana na maguu makubwa ya kushangaza?Suruali wanazozivalia utadhani ni fagio za kufagilia barabara! Vilevile utaona wengine wamezisuka nywele zao. Walio na fupi zisizosikika huzitia dawa kuzifanya ziwe nyororo kama za kizungu. Tangu lini mwafrika mwenye nywele za kipilipili akawa mzungu mwenye nywele za singa? Mbona wavulana wasijivunie Uafrika wa nywele zao?

Bila shaka umewaona wengine waliotoboa masikio na kuvaa herini, vipuli na bali! Wengine wamejaza mikufu shingoni, bangili mikononi na pete vidoleni. Pete hizo zilivyovaliwa, ni vigumu kujua kama wameoa, wamefiwa, wanachumbiwa au wametalikiana! Kila kidole kina pete bila kujali maana yake! Lo! Tunaishi au tunaisha?

Wasia wangu kwa wavulana ni kwamba, wakubali maumbile yao na kuwaachia wasichana mapambo yao. Wakome kujipaka rangi kwenye kucha zao na kukubali asili waliyopewa na Mterehemezi. Kujipamba wafanyavyo wavulana ni utovu mkubwa wa nidhamu na kukosa maadili.

---

41. Mwandishi anapoona mambo ya siku hizi anatamani kufanya nini?
    A. Kuwa mvulana ajipambe kama wao.
    B. Kuuficha uso zake asione uozo ulioko.
    C.Kuwacharaza vijana wanaohusika.
    D. Kuwaelimisha vijana wavae isivyopasa.
42. Msemaji hajaeleza mengi kuhusu wasichana kwani_____
    A. wafanyayo si ibra tena bali kawaida
    B. wasichana wana heshima na taadhima
    C. hataki kuwaaibisha wasichana ilhali hawana doa
    D. hana shida na msichana yeyote mtaani.
43. Ni kipi kinachomduwaza mwandishi?
    A. Kadhia zitendwazo na wavulana hasa.
    B. Mambo yatendwayo na vijana.
    C. Uozo wa kijiji chao.
    D. Vijana wa siku hizi.
44. Ni vitu vingapi vifanywavyo na wavulana na ambayo vinamwudhi mwandishi?
    A. Vitano. B. Sita.
    C. Saba. D. Vinne.
45. Mtu anayeacha desturi za jamii yake na kuchukua nyingine atapigiwa methali gani?
    A. Hewala haigombi
    B. Mwacha mila ni mtumwa
    C. Mkataa wengi ni mchawi
    D. Usiache mbachao kwa msala upitao.
46. Chagua kisawe cha neno Mterehemezi.
    A. Dayani
    B. Bayani
    C. Ahali
    D. Ajinabi.
47. Unafikiri ni nini kimechangia kuwapotosha wavulana?
    A. Utamaduni wa wavyele.
    B. Teknolojia za kisasa.
    C. Elimu nyingi wanayopewa.
    D. Mazingira ya mjini.
48. Wote hawa huvaa pete fulani. Nani asiyestahili kuvaa pete?
    A. Mtaliki.
    B. Mfaruko.
    C. Mchumba.
    D. Mdaiwa.
49. Ni pambo lipi lisilovaliwa shingoni?
    A. Koa.
    B. Kidani.
    C. Mkufu.
    D. Nembo.
50. Kichwa kifaacho ufahamu huu ni
    A. Starehe za kukata na shoka
    B. Ulodi wa maadili
    C. Uongofu wa wavulana
    D. Upotovu wa vijana wavulana.